



# SALA ZA SIKU KENDA

## kwa maombezi ya Albert Joubert na wenzake, wafiadini

Kijitabu hiki kidogo si mkusanyiko wa sala mbalimbali. Novena ni kama sala moja, inayopashwa kuigwa kila siku, kwa siku kenda. Novena ni kama mapigo ya moyo yanayojirudia kila mara. Yesu alisema kama maneno mengi ni bure katika sala… bali ni lazima sala iongozwe na moyo unaodumu kwa upendo.

Kila siku tunamwomba Bwana neema ya pekee. Tuongozwe na Neno la Mungu na tusikilize jinsi mfano wa maisha ya wamisionari wanne unavyoweza kutusindikiza katika maombi. Kwa Enjili na kwa kutoa ushuhuda wa undugu kati ya waamini wao, walitoa maisha yao huko Baraka na Fizi (Uvira, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) mnamo Novemba 28, 1964. Walitangazwa kuwa wenye heri huko Uvira mnamo Agosti 18, 2024: Albert Joubert, Vittorio Faccin, Luigi Carrara, na Giovanni Didonè.

Tufikirie mahitaji yetu na nia za ulimwengu mzima. Tumalizie sala ya kila siku kwa kuomba maombezi ya mashahidi wanne wa undugu.

Wamissionaryo Waxaveriani
Roma, 2025
postulazione@saveriani.org

# Siku ya kwanza

*Neema ya kusali*

Somo fupi Waroma 12, 1-2

Ndugu zangu, nawasihi, kwa ajili ya huruma yake Mungu: mutolee miili yenu kuwa sadaka takatifu, yenye uzima, yenye kumpendeza Mungu: ndiyo ibada yenu ya kiroho. Msishike mwendo wa dunia hii, bali mgeuke kuwa watu wapya, wenye mawazo wapya, mpate kutambua mapenzi ya Mungu, mambo gani ni mema na yenye kumpendeza na makamilifu.

Tufikiri pamoja na Wafiadini wetu

"Barua kwa wazazi" ya Vittorio Faccin, mtawa na shaidi
(*Épistolaire*, Roma 2024, 189; Baraka, 22.11.1964)

*Mashahidi wapya: waombezi wetu*

Siku sita kabla ya kuuawa, frera Vittorio Faccin aliandika:

"Natumaini kama barua hii iwafikie. Afya ni njema japo magumu machache, ambayo yameishapita. Kwetu sasa hakuna ginsi ya kupashana habari: tunaona kiu ya uhuru, lakini uhuru huo utafika wakati gani? Kila siku ni siku ya kungoja. Kuelezea

yale tuliyoyaona wakati huu haiwezekani na yatabakia moyoni mwetu sikuzote.

Mama wa Mbinguni aliyetukinga mpaka sasa kwa mwujiza, ataendelea kutukinga. Naona hakika kwamba tutatokamo salama. Sala zenu zapokelewa mbinguni. Muzidi kusali kwa ajili ya watu hawa wanyonge. Mutoe machozi miguuni mwa Mama wa mbinguni, Mama wa Mitume. Musali. Nawakumbatia wote".




*Albert alikuwa akisoma Misa, akitolea mahitaji ya watu wote; Vittorio alizoea kusali rozaryo wakati wa safari zake; Giovanni alikuwa amejitolea kabisa kwa Bikira Maria; Luigi alikufa baada ya kuungamisha mtu aliyetubu…*

## Bwana Yesu, unifundishe kusali

Niliamini. Niliwaamini.
Niliomba. Niliwaomba.
Niliinua sauti yangu ili nisikilizwe.
Niliwaita kwa majina yenu,
Albert, Giovanni, Vittorio na Luigi.
Niliomba baraka zenu.
Nilibariki majina yenu.

Bado sijaona jibu la Mungu.
Sijui ginsi ya kuomba.
Ili yote yasiwe bure,
ninakuomba, ee Bwana,
ugeuze maombi yangu maskini
kuwa upendo unaotolewa kwa wale wanaohitaji.

Ee Bwana, unifundishe kusali.
Mambo mengi sana yananifikia maishani mwangu.
Unajua! Unaweza! Ninakuamini.
Furaha kubwa kukaa pamoja nawe.
Imarisha ndani yangu neema ya unyenyekevu
na ya majitoleo katika sala.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya pili

*Neema ya msamaha*

SOMO FUPI Wafilipi 3, 7–8

Ndugu zangu, yaliyokuwa faida kwangu, naliyaona kuwa upotevu kwa ajili ya Kristu. Na kweli naona mambo yote ni upotevu, nikiyafananisha na faida kuu ya kumjua Kristu Yesu Bwana wangu. Kwa ajili yake yeye, nimependa kupotelewa na yote nikiyaangalia kama takataka, ili nimpate Kristu.

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo kutoka kitabu cha maisha ya Wenye heri
Albert Joubert na wenzake, mashahidi
(Lisa Zuccarini, *Heureux êtes-vous*, Rome 2024, p. 189)

*Muuaji anaomba msamaha na anaongoka moyoni*

Mara tu baada ya mauaji ya Frera Vittorio na Padri Luigi, miili yao ilikatwakatwa vibaya. Hasa, mkono wa Frera Vittorio viliendeshwa kwa kuonyesha ushindi na kuzunguka kijiji cha Baraka na kijana mlinzi ambaye utambulisho wake unajulikana. Miezi michache tu kabla ya matukio ya siku hiyo, kijana huyo alibadili dini, akawa Mkristu na kuomba kubatizwa. Aliishi Baraka, ambapo

aliendelea kuwa hai sana katika kundi la waamini, akichaguliwa mwongozi wa shirika huko Kalundja.

Wamisionari waliofika katika parokia ya Baraka miaka ya 1970 walimfahamu. Walijua hadisi ya maisha yake na safari yake ya imani. Walimkaribisha katika Eklezya, wakikubali toba yake bila kumchukulia kama mtu wa kuazibishwa. Ombi lake la rehema lilikubaliwa kwa urahisi, kwa sababu kila aliporudi Baraka, alikuwa akisikitika moyoni akisema: "Ndiyo, tuliwaua watu wasio na kosa, watangazaji wa Enjili. Nilitenda vibaya kwani nilifuata sheria wa Wamulele nikisirikia, bila sababu, mwendo ya wakristu." Ujinga wa ujana wake wakati huo ulifunga mawazo yake. Kwa sababu ya majuto yake, hakuna mtu ambaye angemsumbua tena au kudai majibu kuhusu maisha yake ya zamani. Alikuwa alishageuka: na leo angali mkristu mkatolika.

«Ee Bwana, ondoka kwangu,
kwa maana mimi ni mtu mwenye zambi »
(cf. Lk 5,4-8).

## UNISAMEHE, EE BWANA

Wapendwa mashahidi wenye heri,
labda sijawajua bado,
lakini naomba mniombee.

Zambi yangu iko daima mbele yangu.
Nimeua kwa namna mbalimbali, mimi ni mkorofi,
Mimi ni mwoga na mnafiki,
Sijapenda sana, katika maishani yangu.
Sina imani ya kutosha katika Yesu Kristu.
Lakini kwa kweli sina msaada mwingine
maishani mwangu ijapokuwa kwake Yesu.

Ninamwomba Mungu Baba anisamehe
na kuondoa maumivu makubwa
yanayonilemea moyoni.
Bwana anajua uzaifu wangu: anitie nguvu.
Ninaomba msaada wa Bikira Maria,
wa Mtakatifu Yosefu, wa Malaika Mlinzi wangu.
Nawaomba ninyi pia,
Wenye heri mashahidi wa udugu.

Mnisaidie kupata faraja.
Mwokoe maisha yangu na maisha ya wale
wapendwa wangu.
Mungu aikaribishe roho za marehemu wetu.
Aksanti kwa kila kitu na kwa kile mtakachofanya.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya tatu

*Neema ya kuongoka moyoni*

SOMO FUPI Fil 4, 8.9b

Ndugu zangu, fikirini mambo yote yaliyo kweli, yote yaliyo heshima, yote yaliyo haki, yote yaliyo safi, yote yaliyo mapendevu, yote yaliyo na sifa njema, yote yaliyo na fazila na ya kusifiwa. Mambo yaliyofundishwa nami na kuyapokea kwangu, na kuyasikia na kuyaona katika mwendo wangu, fanyeni hayo. Naye Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi !

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo katika Hadisi ya maisha ya Albert Joubert,
Padri na Shahidi
(Emilia Flocchini, Albert Joubert, http://santiebeati.it)

*Utiifu na Mapendevu: fazila mbili za Albert Joubert*

“Katika mwendo wa ya kuiendea Upadirisho, Albert alitumika sana juu ya tabia yake, kwa kuigeuza kuwa nyenyekuvu na ya kufaa. Alijulikana kama mwana wa Kapiteni Joubert, lakini heshima ya watu ilikuwa mbali na moyo wake; yeye

alitamani kukomaa katika utii na katika hamu ya kuleta mafaa kwa wengine.

Baada ya kupadirishwa, tarehe 6.10.1935, Padri Joubert alijiweka tayari kuenda katika missioni za mbali zaidi. Kwanza alitumwa Kasongo, 750 Kilometri mbali na Baudoinville. Halafu alitumika katika missioni mbalimbali nane. Kwa kufika katika miji ya mbali zaidi, alitembea na miguu siku nyingi na hivi apate kuwaletea Masakramenta, kuwafundisha zaidi wakatekista katika elimu ya enjili na kuwapa moyo wa kujitolea. Alipotumwa katika seminari ndogo ya Lusaka na ya Mungombe kuwa mwalimu, alikuwa tayari kusaidia wenzake Mapadri, katika kazi ya kitume, hasa pa nyakati za nguvu zaidi kama vile majilio na kwarezyma. Na popote fazila ya pekee yake ilikuwa roho ya urafiki na ya mapendevu kwa ajili ya wote: kwa kila mmoja alikuwa anaona heshima".



## EE BWANA, SINA MTU MWINGINE (JN 5,6)

Baba padri Giovanni,
mtazamo wako
unigusa sana,
utulivu wako unaniangazia,

ukarimu wako unanipa ushujaa.
Uniombee kwa Mungu ili niwe mpole na mwema.

Unisaidie nipate furaha
ambayo itajaza utupu mkubwa ndani yangu.
Unisaidie katika magumu ya maisha,
angazia giza la mateso ya kila siku,
utulize malalamiko yangu.

Unitoshe kwenye zoruba
kinachonivuta chini.
Unisaidie kuwa nuru ya Kristu,
mkono ulionyoshwa na mguu mwepesi,
kwa kuwatumikia wengine
katika upole na imani sabiti.

Wagonjwa wetu wapate faraja kwa Mungu
na wapate pia msaada kwa njia yetu.
Uniombee, Mwenye heri Giovanni!

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

Wafuasi wakamkaribia Yesu
na kumwamsha wakisema :
« Ee Bwana, utuokoe ! Tunafariki ! »
(Mt 8,25)

# Siku ya nne

*Neema ya chakula cha kila siku*

SOMO FUPI Mt 7, 7-11

Ombeni, mtapewa; tafuteni, mtapata; pigeni hodi, mtafunguliwa. Kwani kila mtu aombaye apewa; kila atafutaye apata; na kila apigaye hodi, atafunguliwa. Au nani kati yenu, mwanae akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akimwomba samaki, atampa nyoka? Basi, kama ninyi, mlio waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vipaji vyema, je, si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wale wanaomwomba?

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo katika barua ya Mwenye heri Vittorio kwa wazazi wake
(*Épistolaire*, Rome 2024, 76-77 ; Mugeri, 24.07.1960)

*Msibakie bila kufanya kazi*

Nimefika Kongo tangu miezi minane na bado sizungumzi lugha vizuri. Shuruli zangu: nawasindikiza wafanyakazi katika Missioni ya Baraka. Ninawaongoza vijana 350 wanaoingia katika vikundi vya kanisa (Xaveri na Skauti). Wametawanyika katika eneo la kilomita 150. Kuna

makanisa ndogo 60 ndani ya parokia. Tunawafikia baada ya saa chache za kutembea, juu ya milima, kupitia mapori, au kando ya Ziwa Tanganyika katika boti ya zamani. Kuanzia Juni 7 hadi 24, 1960, nilitembelea makanisa hayo pamoja na padri mwenzangu. Daraja yangu ilikuwa kuwachunguza makatekumeni. Hapa, kabla ya kubatizwa, lazima wakamilishe miaka minne ya ukatekumenato na kufaulu mitihani minne. Baada ya mwaka wa kwanza, wanapokea "pagaro" (médaille); baada ya pili, msalaba; baada ya tatu, wanaongezwa kwenye oroza ya watakaobatizwa. Katika kijiji kimoja, baada ya siku yao ya kazi, wachimbaji wa kutafuta madini wanazoea kila jioni kwenda kwa mafundisho ya kidini, yanayotolewa na Mkristu mzee ambaye anaweza kusoma, akisaidiwa na mkatekumeni moja.

Kama mnavyoona, kazi haikosekane. Mkitaka, kuna nafasi kwenu hapa pia. Kwa mfano, huko Baraka, nilipo mimi, wakristu wamekuwa wakisubiri watawa tangu 1950 na bado hawajui watafika wakati gani. Msibaki bila kufanya kazi, kwani Bwana hashindwi kutuonyesha mahali



tunapoweza kumtumikia vema. Msali, msali bila kuacha.

## BWANA, UTUPE MKATE WETU WA KILA SIKU

Mwenye heri Frera Vittorio,
ulizijua jamaa zinazoishi katika umaskini
na katika hali ngumu.
Ulitumia muda wako kuwahudumia ndugu zako,
katika maeneo ya ujenzi
na kutafuta mahitaji ya nyumba zao,
kwa upande wa wafanyakazi
na katika utumishi wa kila siku.
Ulifurahi kuweza kupana kazi kwa wale waliohitaji.

Uwaombee kwa Mungu wasiojua ginsi
ya kutatua matatizo yao ya pesa:
wapate kazi zenye malipo mazuri,
kulingana na sheria na yenye inawaheshimu.
Katika kazi zao,
walindwe kutokana na hatari zote
na wapate kuishi katika amani na utulivu.

Uwaombee ili wote waweze kupata chakula,
elimu, na ginsi ya kutunziwa.
Maisha yao yawe ushuhuda
wa baraka za Mungu.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya tano

*Neema ya ulinzi wa kiroho*

SOMO FUPI Wakol 3, 10-11

Mumevua mtu wa kale na matendo yake, mukamvaa mtu mpya anayeongeza upya wake, kwa mfano wa Mwumba wake. Hapo hakuna tena Mgreki na Myaudi, hakuna aliyetahiriwa na asiyetahiriwa, hakuna mshenzi na Mskite, hakuna mtumwa na mtu huru, bali Kristu ni yote na katika wote.

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo kutoka kitabu cha maisha ya Wenye heri
Albert Joubert na wenzake, mashahidi
(Lisa Zuccarini, *Heureux êtes-vous*, Rome 2024, p. 113)

*Albert, mtoto wa kenda, anarisi imani ya wazazi wake*

Hadisi ya Albert, padri mwema na mkarimu, inaanza na hadisi ya baba yake, Léopold-Louis Joubert, na mama yake, Agnès. Kama mtoto yeyote, Albert ni mwendelezo wa kimwili wa wazazi wake, lakini si hivyo tu. Tangu kuzaliwa, mtoto huyu, ambaye angekuwa padri mkongomani, alipokea urisi mzito, wenye umuhimu mkubwa. Hakika, Léopold Joubert amejulikana katika Afrika Kusini, tangu

mwishoni mwa karne ya 19, kama shujaa, mtu mtakatifu na mjeshi mhodari aliyepinga wafanyabiashara ya watumwa. Sifa yake haina mwisho. Ni ukoo wenye uwezo mkubwa, changamoto isiyo sawa kwa mwana yeyote: Albert angeweza kupondwa chini ya uzito wa urisi huu.

Hata hivyo, baada ya muda, sura ya baba si kizuizi bali utajiri katika roho ya kijana Albert. Albert alichukua vipaji vya baba yake, akavibadilisha kulingana na tabia yake mwenyewe, na akakumbatia urisi wa kiroho, akikua kwanza kama mtu na kisha kama kohani. Lakini alijitengenezea njia yake binafsi, akimalizia kwa tendo kubwa sana: kuuawa shahidi na mfiadini. Mwanafunzi huyo, kimya kimya na zaidi ya matarajio yote, alimfikia na kumzidi baba yake!

## EE BWANA, UTUOKOE

Mwenye heri Albert Joubert,
ulishinda nyakati ngumu
kwani uliamini kila wakati katika fazila ya undugu.
Hata adui, kwako, alikuwa ndugu wa kupendwa.

Leo, nakuomba unisaidie kuwaombea
wale wanaotaka kifo changu,
wale walioniumiza kimakusudi,
wale ambao hawaniongeleshi tena,
wale wamenivuta maishani mwao.

Uniombee kwa Roho Mtakatifu:
ili niwe huru na nisijilipize kisasi
na nipate kutoa msamaha.
Bwana anirehemu
na awasamehe wapendwa wangu
na atujalie amani yake.
Bwana akiwa upande wetu,
hatuna hofu tena.



Mwenye heri Albert, utulinde.
Tunaishi nyakati ngumu.
Wengi wako katika vita
na wanakabiliwa na vurugu kali.
Uijalie nchi yako, Kongo,
iweze kuvumbua tena furaha ya undugu:
Bwana awaangazie watu wa vita
na kuwabadilisha kuwa watu wa amani.
Silaha zinyamazwe
na wakubwa wa nchi walinde uzuri wa uumbaji.

Tunajitolea kwako na kwa wenzako.
Natamani, kama wewe,
kuishi na kufa kwa ajili ya Kristu
aliyetaka sisi wote tuwe ndugu.
Aksanti kwa kupokea, bila sifa yoyote,
heshima na utume wa watoto wa Mungu
na wa ndugu wa ulimwengu wote.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya sita

*Neema ya uzazi*

SOMO FUPI 2 Wakor 1, 3-4

Atukuzwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristu, Baba mwenye huruma nyingi na Mungu wa kitulizo cha kila aina. Maana anatutuliza katika taabu zote, kusudi tuweze nasi kuwatuliza wenye taabu mbalimbali, kwa kitulizo kile tunachopewa na Mungu sisi wenyewe.

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo katika utangulizi wa kitabu cha barua ya Mwenye heri Giovanni Didonè
(*Épistolaire*, Rome 2024, 5-6)

*Jamaa zilizo na mizizi katika imani*

Tukiangalia vema jamaa za mashahidi wetu wanne, tunaona utakatifu mkubwa. Wazazi wenye watoto wengi na wenye kuwa na maisha ya mfano. Waliishi wakiangaziwa na Enjili. Watu wasio na umuhimu mkubwa katika mji, lakini wenye mizizi mirefu kwa kusimama imara. Wazazi wa Giovanni Didonè walikuwa na watoto kumi na mmoja. Walipendana kwa undani, bila shaka, bila kuvunjika. Walikuwa na Mungu katika mwili na damu yao,

katika imani iliyowalisha. Angelo Didonè na Maria Marchetti waliwalisha watoto wao mkate wa kimwili na fazila za kiroho. Walifahamu vizuri ya kwama Mungu hamwachi mtu yeyote, kwamba Mungu anatenda ginsi ajabu, na kwamba Mama Maria, akiwa na vazi lake kubwa la mama, anatulinda sote katika mitego mikali ya shetani. Kupitia imani hii ya msingi, Angelo anakomalisha watoto wake, mmoja baada ya mwingine, wakiungana wote pamoja. Baba Angelo anafikiria kazi na sala; Maria "anaweka kila kitu, anayafikiri moyoni, anayapekua na anafurahia kimya kimya" (Barua kwa Dada Tecla, Aprili 13, 1959). Hivyo, watoto kumi na mmoja hupata wito wao wenyewe. Wavulana watatu wanakuwa mapadri (kati yao Giovanni), wasichana wanne wanakuwa watawa, na wanne wanaoa, wote wakiunda jamaa nzuri ambazo huwapa sio tu msaada wa kimwili, lakini zaidi wanahimizana kiroho. Haiwezekani kutosaidiana.

## Ee Bwana, nipate kuona!

Enyi wafiadini wenye heri,
Mmwombee mume wangu (mke wangu):
upendo wetu ubarikiwe
na ubaki imara wakati wa shida.
Mwaombee watoto wetu:
mwalinde katika mawazo yao na matendo yao.

Hasa nawatolea binti zangu:
waleeni katika upendo wa Yesu
na wajue kushukuru kwa hilo.
Mwalinde wale walio na mimba:
mwaokoe kutoka hatarini yote.

Kama Bartimeo, ninawasihi,
ninyi mlio karibu na Yesu:
wapeni wenyi ndoa wakristu
watoto wanaowatamani.
Sikilizeni kilio cha wale wanaotaka
kuwa (au kuwa tena) baba na mama.
Bwana awatimizie mahitaji yao.
Ninyi ambao mmekuwa na jamaa kubwa,
mnajua mzigo unaolemea nyoyoni
ya wenyendoa hao wanaotamani watoto.

Nawasihi, wenye heri wapendwa,
msiniache kimya kimya.
Kwa Yesu, mambo yote yanawezekana.
Njoo, Roho Mtakatifu,
uifanye upya moyo wangu,
niongoze popote unapotaka nihudumie.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya saba

*Neema ya uponyaji*

SOMO FUPI Waroma 8,28.35.37-39

Twajua ya kama mambo yote yaleta mema kwa wale wanaompenda Mungu, ndio wale walioitwa kadiri ya kusudi lake... Nani atatutenga na mapendo ya Kristu? Ati ni taabu , ao misongo ya roho, ao mazulumu, ao njaa, ao uchi, ao hatari, ao upanga?...Lakini mambo hayo yote tunayashinda kabisa kwa nguvu yake yeye aliyetupenda. Nina hakika kama wala mauti, wala uzima, wala Pepo, wala Watawala, wala mambo ya sasa, wala mambo yatakayukuja, wala Wenye uwezo, wala Nguvu za juu, wala za chini, wala kiumbe chochote kingine, hakitaweza kututenga na mapendo ya Mungu, katika Kristu Yesu, Bwana wetu.

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo katika barua ya Mwenye heri Vittorio kwa binamu Viktorina
(*Épistolaire*, Roma 2024, 171; Baraka, 26.12.1963)

*Kudumu tukitenda mema ni alama ya mapendo maaminifu*

"Dada mpenzi,

Bwana anataka tena kupima mapendo yako kwa ajili yake. Katika majaribu hayo, uwe hodari, vumilia yote katika mapendo yake ili neema nyingi zishuke juu ya jamaa yako, hasa juu ya watoto. Hakuna waridi bila miiba. Katika waridi, tafuta tu uzuri na harufu tamu: uzuri na harufu zakusahaulisha mapigo ya miiba. Maisha yetu kwa ajili ya Yesu yapashwa kuwa mapendo tu. Bwana anataka roho yako iwe nzuri zaidi, safi zaidi, mtakatifu zaidi, labda kwa hiyo amekuitikia mateso na mapendo. Hivi amekupa wakati wa kusali na kufanana naye kila siku zaidi.

Mimi nitakukumbuka wewe katika sala zangu, pamoja na mume wako na waana wako, ili nao wawe na nguvu ya kuvumilia yote kwa mapendo ya Yule Mungu aliyejifanya mtu kwa kutujua na kutupenda zaidi. Naungana nanyi katika Yesu na Maria Mama wa mbinguni".



## UTUOKOE KATIKA MAOVU

Mwenye heri Luigi, shahidi.
Ulipokuwa mtoto,
Bwana alikuokoa
katika ugonjwa mkali.
Mama yako alizani utakufa.
Ombi lake lilijibiwa.

Uwaangalie leo wagonjwa wetu wote,
hasa wale tunaowaombea siku hizi.
Kwa mfano, mtoto huyu wa miaka 11,
mtoto pekee,
aliyelazwa hatarini hospitalini.
Siku moja, alimwambia mama yake:
"Nilimuuliza Yesu kwa nini
mimi na watoto wengine tunagonjwa.
Nilielewa kwamba mara tu nitakapopona,
nitajua ginsi ya kushukuru kwa kila jambo."

Bwana yuko kweli katika maisha yetu,
kama vile alivyokuwa pamoja na wafuasi baharini
ndani ya mashua yenye msukosuko mengi.
Mioyo yetu inalia.
Mwenye heri Luigi, utuombee kwa Mungu.

Kati ya wagonjwa wetu,
kuna wanaokuwa taabani, katika hatari ya kufa:
wafarijikwe na watu wanaoungana nao.
Mwenye heri Luigi,
unisaidie kumtolea Mungu ugonjwa wangu
na uzaifu wangu wote
ili niwe mtu wa kuleta matumaini duniani.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya nane

*Neema ya utambuzi*

SOMO FUPI Mt 28,16.18-20

Wale wafuasi kumi na mmoja walienda Galilea mpaka mlima ule walioagizwa na Yesu... Yesu akawajongea akawaambia: «Nimepewa uwezo wote mbinguni na duniani: basi, nendeni mkafanye mataifa yote kuwa wafuasi, mukiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, na kuwafundisha washike yote niliyowaamuru nyinyi. Na tazameni, Mimi nipo pamoja nanyi siku zote, mpaka mwisho wa dunia.

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo katika barua ya Mwenye heri Luigi
kwa wazazi wake
(*Épistolaire*, Roma 2024, 171-172; Fizi, 11.02.1964)

*Mchoko na furaha katika kutangaza Enjili*

Padri Luigi anahadisia safari yake ya kwanza, safari katika miji ya milima ya Fizi; ilidumu siku kumi.

"Padri Giovanni, kabla ya kuondoka ameniambia: 'Utafika bila nguvu, kama mfu: usiungamishe kwanza'. Lakini namna gani kuwaambia watu 'Hapana sasa'? Walikuwa

wakatekista na wengine wa karibu, walionisihi: ‘Padiri, kesho watu watakuwa wengi sana, watatoka ngambo zote, utakosekana wakati: utuungamishe sasa’. Niliitika. Bila kubadilisha hata nguo zenye kujaa jasho, nilikamata kiti, kila mwamini akipiga magoti juu ya udongo, tumeanza. Walikuwa wachache na pa saa moja na nusu ya usiku (19h30) wameniacha. Mimi nimetokotesha, katika chungu kidogo, maziwa waliyonipa. Halafu ningalitamani kusali na baadaye kulala usingizi. Lakini pa saa mbili ya usiku (20h00) wamegonga mlangoni. Ni wajirani wanaoshika nafasi ya kuongea na Padri, na kuuliza habari nyingi... Wameniacha pa saa tatu na nusu ya usiku (21h30). Ndipo natimiza mambo yangu na kulala”.

## BWANA, UNATAKA NIFANYE JE?

Wenye heri Giovanni, Vittorio, Albert, Luigi,
mlitambua mapenzi ya Mungu katika maisha yenu.
Nawatolea ninyi watoto wetu vijana:
washinde wakati wao wa upinzani,
wapate njia ya kweli ya maisha
ili kumpenda Mungu na kuwatumikia ndugu zao.

Nawatolea ninyi wanaochumbiana:
wajue ginsi ya kupendana kikweli,
bila unafiki wala mazoezi mabaya.

Mwaombee vijana wenye uwito
wa kipadri na ya kitawa:
wawe huru kwa kushinda vishawishi,
waishi katika unyenyekevu, usafi na utii,
wajitolee katika upendo,
tayari kuzoea maendeleo mapya ya Eklezya.

Wenye heri wafiadini,
mlitolea maisha yenu kumtangaza Kristu,
nawaomba mrudishe mume/mke wangu,
watoto wangu, wazazi wangu kwa Yesu.
Wale waliomwacha, warudi kwenye imani
na wakutane na Mwokozi wetu.

Mniombee mimi pia:
Bwana anisaidie kupata tena njia yangu,
nielewe kilicho cha lazima kwangu,
niangaziwe ili nitende vema.
Kwa yote mnayofanya,
aksanti na utukufu kwa Mungu.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Siku ya kenda

*Neema ya kazi ya kitume*

SOMO FUPI Eb 13,7-9a

Wakumbukeni waongozi wenu waliowaletea nyinyi Neno la Mungu. Fikirini kwa uangalifu mwisho wa namna yao ya kuishi, fuateni imani yao. Yesu Kristu ni yuleyule jana na leo na hata milele! Msivutwe na mafundisho ya namna mbalimbali na ya kigeni.

TUFIKIRI PAMOJA NA WAFIADINI WETU

Somo katika barua ya Mwenye heri Giovanni
kwa Rafaeli, mkatekista wake

(*Épistolaire*, Roma 2024, 422; Lett. del 09.11.1964)

*Utumishi wa kitulizo: kushurulikia moyo za watu*

“Aksanti kwa barua yako na kwa kazi unayotimiza. Sasa kule Roma, katika mtaguso wa Vatikano, walitoa ruhusa kwa Maaskofu wa missioni, ya kuweka mashemasi wawe wasaidizi wa Mapadri; maana yake Askofu anaweza kuchagua wakatekista wenye maisha ya haki na uaminifu na juhudi, wapate ruhusa ya kubatiza na kukomunisha waamini (…) Hayo nakuandikia kwa kukupa

kitumaini katika nyakati zijazo. Mvumilie kidogo tu na mtakuwa na Shemasi kwenu. (…). Sisi Mapadri tuko hapa Fizi, mbali sana na nchi zetu, lakini Mungu ni popote na anatuangalia. Tukae imara! Msizani kama Mapadri wataenda kwao. Mjue kwamba hao wanapenda kufa kuliko kuwaacha nyinyi. Msisadikie upesi maneno ya wongo. Sisi tumetumwa kwa kubaki hapa, katika missioni ya Fizi. Mimi sifike bado kwenu kwa sababu siwezi, -nyinyi mnajua wazi-. Lakini mtaniona tu, sijui wakati gani, lakini mtaniona tu. Mkae imara".

### WOTE WAWE MOJA

Ee Mungu Baba Mwenyezi,
kupitia maombezi ya wenye heri wa Uvira,
unifanyizie niwe wazi na mkarimu,
hasa kwa maskini, wazee,
wale wasio na upendo,
na wale ambao bado hawajajua upendo wako.

Ninakuomba nguvu na uhodari
wa kuwa mhimizaji wa upendo wako,
wa umoja na imani,
hasa ndani ya jamaa
na kwenye Wakatoliki si wengi.

Ushushe Roho yako
kwa wale wanaoishi katika nchi ya kigeni,

mbali na jamaa zao na nchi yao:
fungua macho yetu kwa mahitaji ya ndugu zetu
panua mikono yetu kwa kushiriki tunayo.

Unifanyizie niwe mwangalifu kwa shida za ndani
za vijana wetu ambao kwa nje
hawaonyeshi magumu yao.
Unifanyizie niwe chombo chako cha upendo.
Unisaidie kuwatumikia kwa furaha
walio wadogo kati yetu.

Wenye heri wapendwa,
nawatolea mapadri wetu:
wajifunze kusaidiana,
washurulikie walio zaifu zaidi,
watende kwa upendo kila wakati!
Damu yenu iliyomwagika iwe matunda
ya kuzalisha wamissionari wengi.

Ee Baba Mtakatifu, uwalinde wamissionari wetu:
uwasaidie waishi kindugu
kwenye mwanadamu anahitaji wokovu wa Kristu
mwana wako mpenzi.

(Tumalizie na Sala ya Maombezi, uk. 30)

# Sala ya mwisho

Tusali kwa maombezi ya Wenye Heri
Albert Joubert na wenzake, wafiadini

Baba Mtakatifu, mwenyi huruma tele,
wewe umeipatia Eklezya yako abbé Albert Joubert
na Waksaveriano Vittorio Faccin,
Luigi Carrara na Giovanni Didonè,
wachungaji na mitume
kadiri ya Moyo wa Mwana wako Yesu Kristu.

Wakiwaka moto wa mapendo,
hawakuacha kundi la kondoo katika hatari
bali walibaki kulilinda mpaka kumwaga damu,
wakishuhudia undugu usio na mipaka.

Kwa maombezi yao, utujalie neema
tunayokuomba kwa unyenyekevu.
Kwa ajili ya Kristu, Bwana wetu. Amen.

Bwana atubarikie, atukinge na maovu yote na kutufikisha kwenyi Uzima wa Milele. *Amen*

Wote wamjue na kumpenda,
*Bwana wetu Yesu Kristu.*

Mt. Guido Maria Conforti na Mt. Fransisko Xaveri, *mtuombee.*

# Oroza

Siku ya kwanza......................................................3
*Neema ya kusali*..................................................3
Siku ya pili............................................................6
*Neema ya msamaha* ............................................6
Siku ya tatu ..........................................................9
*Neema ya kuongoka moyoni* ...............................9
Siku ya nne .........................................................12
*Neema ya chakula cha kila siku* .......................12
Siku ya tano ........................................................15
*Neema ya ulinzi wa kiroho* ...............................15
Siku ya sita .........................................................18
*Neema ya uzazi* .................................................18
Siku ya saba.........................................................21
*Neema ya uponyaji* ...........................................21
Siku ya nane ........................................................24
*Neema ya utambuzi*...........................................24
Siku ya kenda.......................................................27
*Neema ya kazi ya kitume* ..................................27
Sala ya mwisho....................................................30


TÉMOINS DE LA FRATERNITÉ
Baraka et Fizi (Uvira, RD Congo)